# Learning by Ear 2011/2012 – Corruption – The Elephant in the Room

## Episode 03 – "Strong Principles Needed"

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Friederike Müller, Pendo Paul**

**Proofreading: Charlotte Collins, Pendo Paul**

**KISUAHELI: Eric Ponda**

CHARACTERS:

- NARRATOR

Scene 1:

- Jennifer (FEMALE, 55)
- Mr Kitwara (MALE, 45)
- Mrs Mutua (FEMALE, 65)
- NARRATOR

Scene 2

- Sylvia (FEMALE, 19)
- Lydia (FEMALE, 16)
- Alfayo (MALE, 58)
- Jeffrey (MALE, 58)
- Jennifer (FEMALE, 55)

## Intro:

### 0. Narrator:

Hujambo na karibu katika vipindi vya **Noa Bongo Jenga Maisha yako.** Hii ni sehemu ya tatu kwenye mfululizo wa mchezo huu wa redio kuhusu ufisadi kwa jina “**Tembo Nyumbani**” unaozungumzia hali halisi ya maisha. Katika kipindi kilichotangulia rafiki mkuwa wa familia ya Odhiambo, Jeffrey Thiongo, anaachishwa kazi katika Bodi ya kupambana na Ufisadi. Na sababu kubwa ni utendaji kazi duni ambao yadaiwa hauridhishi, lakini Jeffrey anashuku sababu kubwa ya yeye kufutwa kazi ni kutokana na kashfa ya ufisadi, katika sekta ya nishati inayowahusu watu wa ngazi za juu serikalini ,wakiwemo mawaziri na wafanyabiashara mashuhuru. Pia tulisikia jinsi Isaac Odhiambo alivyokamatwa na maofisa wa usalama akiongea na simu huku akiendesha gari barabarani, na jinsi alivyoepuka kufikishwa katika kituo cha polisi baada ya kumhonga ofisa wa polisi .Na anaposimulia familia yake kuhusu kisa hicho, wanamshtumu kwa tabia hiyo. Na katika kipindi hiki cha leo chini ya kichwa, "**Yahitaji Maadili thabiti**", Jeffrey anaamua kuzindua mradi mpya huku Mamake Isaac akikabiliwa na mtihani mkubwa shuleni.

## Scene One:

**1. SFX:** **School kids playing outside in the playground**

**2. SFX:** **Knock at the door**

**3. Jennifer:** Hello, come in.

**4. Mr. Kitwara:** Oh, habari Bi. Odhiambo, tunaweza kukutana na wewe japo kwa dakika tano tu? Ningependa kuwa na mazungumzo nawe kuhusu mtoto wangu, Gitura, na jinsi anavyoendelea na masomo yake shuleni.

**5. Jennifer:** Bila shaka, Bw. Kitwara. Pita ndani na karibu kiti.

**6. SFX:** **Sound of door closing and chair being pulled back**

**7. Mr Kitwara:** Asante. Sitaki kuchukua muda wako mwingi.

**8. Jennifer:** Ni sawa, niko na dakika kama 10 kabla ya wanafunzi kuingia darasani. Kwani una wasi wasi kuhusu matokeo ya Gitura ya mtihani wa mwishoni mwa mwaka?

**9. Mr Kitwara:** Ahhhh… ndio hapana, hapana!

**10. Jennifer:** Sawa. Nimezungumza naye kuhusu matokeo hayo. Hayakuwa mabaya sana. Lakini anaweza kufanya vyema zaidi endapo ataongeza bidii. Nimependekeza pengine aanze kuhudhuria masomo ya ziada katika baadhi ya masomo. Uko tayari afanye hivyo?

**11. Mr. Kitwara:** Mwalimu kama unavyofahamu, Gitura ana kazi nyingi. Anapenda sana kucheza mpira baada ya masomo, na sidhani kama atakuwa na muda huo wa kujiunga na masomo ya ziada. Kwa ushirikiano, naamini tunaweza kupata suluhisho la haraka badala ya kupitia mambo yote hayo.

**12. Jennifer:** Suluhisho la haraka? Samahani lakini sidhani kama kuna njia ya mkato, iwapo kweli anataka kuimarisha matokeo yake.

***KW begins***

**13. Mr Kitwara:** Sasa Bi. Odhiambo, kwani lazima nifafanua zaidi....? Nasema hivi, namaanisha sio kitu unachoweza kumfanyia kila mwanafunzi?

**14. Jennifer:** Hakuna kitu ninachoweza kumfanyia mwanafunzi binafsi mbali na ile kazi yangu ya kuwapa elimu wanafunzi wote kadri ya uwezo wangu na bila kubagua. Hivi una maana gani Bw. Kitwara?

***KW ends***

**15. Mr. Kitwara:** Napendekeza pengine "kitu kidogo" ' kama kiinua mgongo', Unaweza kumsaidia Gitura kuimarisha matokeo yake shuleni! Na kama ulivyosema matokeo yake si mabaya, anachohitaji ni usaidizi na kuongeza bidii kidogo tu. Na nafikiri wewe unaweza kufanya hivyo endapo utapata msaada kidogo kutoka kwangu. Tunafahamu kwamba mishahara ya waalimu iko chini sana!

**16. Jennifer:** Bw. Kitwara, kama unataka kujihusisha na rushwa, basi samahani sana, umekosea jaribu mwengine! Sijawahi na siwezi kula rushwa kwa lengo la kuimarisha matokeo ya mwanafunzi yoyote yule. Haiwezekani na pia ni kuzorotesha

juhudi na uwezo wa mtoto wako kama unafikiri rushwa ndio njia pekee ya mkato kuboresha matokeo yake.

**17. Mr Kitwara:** Lakini nadhani tabia hii imeenea sana shuleni. Rafiki yangu mmoja alishangaa ni kwanini sijawahi kulifikiria suala hili!

**18. Jennifer:** **(anrgy)** Imeenea kote shuleni lakini sio darasani mwangu. Hili jambo lazima niliwasilishe kwa Mwalimu mkuu Bw. Kitwara! Hebu nifuate.

**19. SFX:** **pushes back chair and stands up, walks out of the classroom and up the corridor**

**20. SFX:** **knocks on the door and opens it**

**21. Jennifer:** Habari ya asubuhi Bi. Mutua. Niko na mmoja wa wazazi ambaye ameandamana nami hapa! Anaitwa Bw. Kitwara, babake Gitura. Angependa kuzungumzo na wewe.

**22. Mrs Mutua:** Aaaah, Habari ya asubuhi Bi. Odhiambo ..na Bw. Kitwara! Tafadhali karibuni viti. Ehhe nikusaidie vipi Bw. Kitwara?

**23. Mr Kitwara:** Asante sana Bi. Mutua. Tumekuwa tukijadiliana na mwalimu kuhusu matokeo ya mtoto wangu Gitura, na nakapendekeza apewe usaidizi zaidi katika juhudi za kuimarisha matokeo yake.

***KW begins***

**24. Mrs Mutua:** Kumbe! Na mkaafikiana vipi?

**25. Jennifer:** Nimependekeza Gitura apewe masomo ya ziada, lakini yaonekana Gitura anapenda sana kucheza mpira baada ya kutoka shuleni….

**26. Mr. Kitwara:** Ni kweli anapenda sana kucheza! Hivyo nikapendekeza.. labda kuna njia ya mkato ya kumsaidia ....

***KW ends***

Na naamini unanielewa ninachomaanisha Bi. Mutua...

**27. Mrs. Mutua:** Sawa, labda tunaweza kumssaidia Bw. Kitwara. Binafsi nitachunguza matokeo yake na tunaweza kujadiliana zaidi kesho ukija.

**28. Jennifer:** Bi. Mutua isiwe utakubali hongo ili kumuongeza alama za Gitura! Huo ni ufisadi! Na tabia hiyo haiwezi kukubalika hapa shuleni!

**29. Mrs. Mutua:** **(ignoring Jennifer)** Kama nilivyosema Bw. Kitwara unaweza kunifahamisha tu ni kiwango gani cha msaada anaohitaji Gitura, kisha mambo mengine tutazungumza kesho ukija ofisini.

**30. Mr Kitwara:** Asante sana Bi. Mutua. **(handing over an envelope)**

**31. SFX:** **Envelope being handed over**

**32. Mr Kitwara:** Hii hapa ni zawadi kidogo. Nilijua wewe ungeweza kunielewa na kumsaidia mtoto wangu Gitura. Tutaonana Kesho! Asante sana kwa muda wako.

**33. SFX:** **door opening and closing**

**34. Mrs. Mutua:** Oooh Bi. Odhiambo unashangazwa na nini! Kwani hii ni mara yako ya kwanza kuona mambo haya yakifanyika? Basi, umekuwa ukikosa pesa nyingi sana! Napendekeza ufumbue macho ili unufaike kama wengine. Siku njema!

**35. Jennifer:** Ni kweli Bi. Mutua ninashangaa sana! Nilikuwa na imani kubwa sana kwako kama mtu anayeweza kuwa kielelezo na mfano wa kuigwa. Nilitarajia kuonyesha mfano mzuri kama mwalimu mkuu.Mimi sina nia ya kuwa kama wenzangu. Kujipatia pesa kupitia mbinu hizi za ufisadi. Na najivunia sana kuwa Mwalimu anayefanya kazi yake inavyostahili kuhakikisha wanafunzi wanafaulu kutokana na bidii zao! Sivinginevyo! Siku njema pia!

**36. SFX** **door slamming shut**

**37. Narrator:** Bi Jennifer anaona kama vitimbi. Na ni tatizo linalowakuta wengi, na kujikuta katika njia panda- kudumisha madili mema au kuchukua njia ya mkato na shiriki rushwa! Rafiki ya Bw Odhiambo tayari amekata kauli.

## Scene Two:

**38. SFX:** **Cooking, table being laid, tv on in background**

**39. Alfayo:** Jeffrey, ni vizuri umefika. Ni muda mrefu tangu ututembelee na kujumuika nasi kwa chakula cha jioni.Pengine tutakuwa tukionana mara kwa mara baada ya wewe kuacha kazi! **(chuckles)**

**40. Sylvia:** Baba, usiseme hivyo.Jeffrey unapitia wakati mgumu sana baada ya kisa cha kuachishwa kazi.

**41. Jeffrey:** Asante sana Sylvia babako hana huruma kabisa! **(laughing)**… Lakini pengine ni kweli anayoyasema!. Ile kazi ilikuwa inachukua muda wangu mwingi maishani.. ..na sikuona ni kwa faida gani?

**42. Lydia:** Lakini ulikuwa na imani kwa kazi uliyokuwa ukifanya?

**43. Jeffrey:** Ndio Lydia., bila shaka. Hadi wakati nilipotambua kwamba, kesi za ufisadi hazichunguzi au mara nyingi kuzimwa kabisa.

**44. Jennifer:** Unamaana zinapuuzwa?

**45. Jeffrey:** Ama kwa hakika Jennifer,kila mara wakubwa wangu hutoa visingizio eti kesi za aina hii haziwezi kuchunguzwa kutokana na gharama,mara hakuna ushahidi wa kutosha au mara nyingine ushahidi umepotea. Mambo haya yanafanyika sana.

**46. Sylvia:** Kwa hiyo baada yakufahamu kuwa mambo yanakwenda kombo... kwanini hukutoa habari kwa maofisa wa ngazi za juu zaidi?

**47. Jeffrey:** Sylvia, tatizo ni kwamba wakubwa wengi katika halmashauri hii ni wahusika wakuu, akiwemo mwenyekiti.

**48. Sylvia:** Kweli?

**49. Jeffrey:** Nasikitika sana. Nilifahamu hivyo wakati aliponiachisha kazi. Na chanzo cha yote hayo ni ile kashfa katika sekta ya nishati. Nina uhakika Bw. Alfayo, ungependa sana kusikia zaidi kuhusu suala hili, maana linaigusa kazi yako moja kwa moja. Baadhi ya wanasiasa mashuhuri wamekuwa wakitoa kandarasi bandia za huduma za umeme. Na nyingi ya kampuni zinazopewa kandarasi hizo kutoa umeme ni bandia! Nashuku wanasiasa hawa hatimaye, ndio wanaofaidika na pesa hizi. Pengine hata Rais pia ni mhusika!

**50. Lydia:** Na tangu ulipofahamu haya, umechukua hatua gani Jeffrey.

**51. Jeffrey**: Mara kadhaa nilijaribu kumweleza mwenyekiti. Lakini kila mara faili za kesi hizo hutoweka ghafla. Na ndipo nikaja kufahamu ni kwanini! Nafikiri hata huyo mwenyekiti wa halmshauri ya kupambana na ufisadi ni mshirika mkuu! Wanasiasa hao wanamlipa pesa nyingi asiweze kuendelea na uchunguzi wa kesi hizo. Lazima anapewa kitu kidogo.

**52. Sylvia:** Ndio sababu wakakuachisha kazi- ili iwe rahisi kwao kuendeleza uovu wao huo bila ya pingamizi au kuulizwa maswali.

**53. Jeffrey:** Hasaa, Sylvia. Lakini sitakoma ng'o! Lazima nitaifichua kashfa hii - hasa wakati huu uchaguzi unapokaribia.

**54. Jennifer:** Kwani usianzishe shirika lako la upelelezi dhidi ya visa vya ufisadi nchini? Na hakika utapata msaada mkubwa kutoka kwa mataifa wafadhili. Na watu hapa watakuunga mkono. Jaribu!

***KW begin***

**55. Lydia:** Mama hilo ni wazo zuri sana. Jeffrey lazima uanzishe shirika lako. Kwani sasa hivi utakuwa ukifanya nini? Hawa hawawezi kukuajiri tena ikiwa wanajua kwamba utakuwa pingamizi katika shughuli zao.

***KW ends***

**56. Jeffrey:** Ni kweli si wazo baya Jennifer. Nafikiri nitaanza kushughulikia suala hilo mara moja.

**57. Sylvia:** Mimi nitajitolea kukusaidia! Nitatuma maombi ya kujiunga na chuo kikuu na nadhani itanisaidia kupata ujuzi zaidi.

**58. Jeffrey:** Kweli naweza kukuajiri kama msaidizi wangu Sylvia! Wacha nitalifikifikiria, nyinyi mlinifanya nikafutwa kazi! **(laughing)**

**End of scene**

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**59. NARRATOR:** Na hadi hapo tunafika mwisho wa kipindi cha leo kwenye mfululizo wa mchezo huu wa redio kuhusu jinamizi ufisaidi. Jeffrey amejitolea kuhakikisha kuwa kashfa kuhusu sekta ya nishati inafichuka- lakini rafiki yake Alfayo atakuwa amemweka wapi? Kumbuka, kampuni yake inahusika moja kwa moja, bila yeye mwenyewe kufahamu. Kama umekuwa ukifuatilia kwa makini, uligundua kwamba Alfayo hakuchangia chochote wakati wote Jeffrey alipokuwa akizungumzia kashfa hiyo ya niishati? Ungana nasi tena kwa kipindi kinachofuata ili upate kufahamu zaidi jinsi ufisadi unavyoathiri maisha ya jamii. Ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu wa dw.de/lbe. Au pia, kututumia maoni kupitia ukurasa wetu wa Facebook. Hadi wakati mwengine tutakapokutana tena. Kwaheri kwa sasa.